

TAREKH YA AMU

BY

AHMAD MOHAMMAD AL-JAHDHMY

KWAJINA LA MWENYEEZZIMGU NITAANZA LEO 28th MARCH 1968 kueleza
KHABARI YA TARIKH YA KISIWA CHA LAMU NA WATU WAKE.

MIMI SASA NIMEFIKA AMA NITAFIKA KWA KUKURUBIWA KUINGIYA UMRI WA MIAKA 58. NILIZALIWA 6th APRIL 1910. BABANGU ALIKUFA KANIACHA YATIMA MWENYE UMRI WA MWAKA M'MOJA NA MIEZI MINANE TU NILILELEWA NA MAMANGU NA ALIFANYIZA WAJIB WAKE KWA KUNISOMESHA QURANI NA ILIMU YA DINI YA KI ISLAMU. ALHAMDULILLAHI NAMSHUKU M'GU KWA TAUFIKI YAKE.. NAMUOMBA M'GU AMRAHAMU MAMANGU. BABANGU SIKUMUONA ILLA NIMEMUONA KATIKA PICTURE TU. YA RABBI MRAHAMU MAMANGU KAMA SURA ALIVONILEYA MIMI KATIKA UTOTO WANGU.
KADHALIKA NAMUOMBA M'GU AMRAHAMU NA BABANGU INGAWA HAKUDIRIKA KUNILEYA KWA SIKU NYINGI LAKIN ALIUSIYA KABLA YA KUFA AKIFA NIHAFIDHISHWE QURANI. MAMANGU ALITIMIZA WASIYA WAKE.. MAALASAF NILIWAHI KUHAFIDHISHWA JUZUU KUMI NA TANO TU MAALIM WANGU HAMID ALIKUFA NA SIKUENDELEYA KUHIFADHI.. YARABBI WARAHAMU BABANGU? NA MAMANGU? NA WAALIM WANGU YEYE NA NDUGUYE MAALIM AHMAD WALIOKUWA WAKISOMESHA PAMOJA..
NILISOMA MUKHTASARI WA ILMU ZA DINI YA KIISLAMU KWANZA KWA ALIMULALLAMA HABIB MANSWAB BIN ABDULRAHMAN AL- HUSAINY. BAADAE KWA HABIB AHMAD BADAWY BIN SEYYED SWALEH?. BAADAE KWA HABIB MOHAMAD ADNANI AL-AHDALY? NAPIYA KWA WAALIM WANGU HAMID NA AHMAD BIN ABDULLA AL-ANJAZINJY. M'GU TAWARAHAMU ATUNUFAISHE KWA BARKA ZAO NA ILIMU ZAO ATUTIYE PEPONI PAMOJA NAWAO.AMIN.
NILIPOKUWA MTU MZIMA NILI INGIYA SCHOOL YA USIKU. MCHANA KIFANYA KAZI KWA MACKENZIE. BAADAE NILIACHA KAZI KWA MACKENZIE KAFANYA KAZI YA UALLIM KATIKA SCHOOL YA USIKU.. BAADAE KAWA NI MWALIMU KATIKA SCHOOL YA MCHANA YA SIRIKALI.. MPAKA MWAKA 1959 KABADILISHWA KAPEWA KAZI YA MUDIRI(D.O.) NILIPELEKWA KIUNGA. NILIKAA KIUNGA MIAKA MITATU UNUSU. BAADAE NILIKWENDA MACCA KUHIJI NA MADINA KUMZURU SAYYEDINA MOHAMAD SWALALLAHU ALAIHI WASALLAM KATIKA MWAKA 1961. NILIPORUDI MACCA NILIPELEKWA WITU KWA KAZI ILEILE YA MUDIR.. MWAKA 1964 NILIRETIRE. SASA NAPATA PENSION. NAMUOMBA MOLA WANGU ANISAMEH MAKOSA YANGU NILIOKOSA NANILIO FANYA KWANI MWENYEEZZIMGU NIMUWEZA WAKUGHUFIRIYA MADHAMBI YOTE MAKUU NA MATOTO KWA REHMA ZAKE KUNDUFU.

KATIKA MAISHA YANGU NIMEONA WAKE WAWILI M'MOJA NILIZAA NAE WAPILI HAKUZAA KWANGU. MOLA MENIRUZUKU WATOTO WAWILI WANAUME NAWATOTO SITA WANAWAKE.. YARABBI NIWEKEYA NA UWAONGOZE KATIKA NJIYA NJEMA WAWE NIWENYE KUFUATA NJIYA YA DINI YAKO YA HAKI WAO NA DHURIA ZAO.AMIN

UJANANI MWANGU NILIKUWA MAISHA YANGU KIPITISHA NUMBANI KWA MAWANGU NAKIPENDA KUKAA NA BABU YANGU BWANA MAAWIYA NAMAKHALI ZANGU.. NAKUPENDA KUSIKILIZA MAZUNGUMZO YAO(MAONGEZI) NAKWENDA SHAMBA KILA LAASIRI ILI KULIAMIRISHA SHAMBA NILILOKUWA NIMEACHILIWA NA BABANGU LA (MSUMARINI).

MSOMAJI

NIMEONA NI BORA KWA FAIDA YAVIZAZI NA VIZAZI VA SIKU ZIJAZO NIELEZE HAYA MACHACHE NIYAFAHAMUYO WILIO YAPATA KWA WAZEE AMBAYO YANA UKWELI NA SAWA KATIKA TAREKH YA LAMU NA WATU WAKE. WAPO WATU WENGI WATOLEYAO KHABARI ZA LAMU AMBAZO HAZIFUATANI NA TAREKH YA KWELI YA LAMU. MWISHO ITAPOTEYA KABISA. LAKIN NATUMAI KWA FADHLI ZA M'GU WENGI WATAFAIDIKA KWAKUISOMA TAREKH HINI. KWAKUWA NIYAKWELI NA YASAWA. MIMI MWENYEWE NIMEZALIWA LAMU. NALIINUKIYA KUPENDA KUKAA NA WAZEE(YAANI WATU WAZIMA)) NAKUSIKILIZA MAONGEZI YAO NA KHABARI ZAZAMANI. KWAHIVO NIMEKULIA KUJUWA MENGI KUTOKANA NA WAZEE NDIYO KAPENDA FAIDA HINI NILIOPATA MIMI IENDELEE VIZAZI KWA VIZAZI NA M'GU TANIWAFIKIYA NIITIMIZE(AMIN).

SASA NITAANZA KUIELEZA LAMU NA WATU WAKE.

LAMU NI KISIWA CHA MCHANGA MWEUPE NA KIZURI KILIOPO KATIKA BAHARI YA INDIAN OCION.. KUTOKA MOMBASA NIKIASI CHA MAILI 164 KWA BAHARI NA MAIL KIASI 225. KWA NJIYA YA BARA. ARDHI YAKE YAFAA SANA KWA MINAZI. MIBIBO(MIKOROSHO) NAPIYA NI MAARUFU SANA KWA MAEMBE YA KISIWA CHA LAMU KINA MILIMA YA MCHANGA MWEUPE NA UFUWO BAHARI MZURI SANA WENYE MCHANGA MWEUPE. KISIWA CHA LAMU KINA MAJI MEMPOPOTE UNAPOCHIMBA UTAPATA MAJI TAMU.

WAKAZI WAKE WENGI WANAOISHI KISIWANI HUMU NI WA ISLAMU.

WAPO MAKABILA MENGI MBALIMBALI WANAOISHI KISIWANI HUMU. KAMA: WA ARABU. BAJUNI. WA AFRIKA.WAZUNGU.WAHINDI NA WAASIA WENGINE

SASA NITAANZA TAREKH YA LAMU.

ASILI YA WATU WA LAMU NI WAARABU WALIOTOKA UPANDE WA DIMISHKI ASHAM(SYRIA) ALIEWALETA NI ABDULMALIK BIN MARWANA. KHALIFA WATANO KATIKA EZZI YA BANU UMAIYYA. KAMA INAVO ONESHA KATIKA KITABU CHA TAREKH(UMMEYYADS) A.H.. 65-86.(A.D.) 685-706.. INGAWA ALIWAKUTA WAARABU WENGINE WALIOTANGULIYA KUWEPO WALIOKUJA KUTOKA(MAKAMKUN) ANNUHAS 2 KWA MUJIB WA RECORD ZA SWAHILI KHALIFA ABDULMALIK BIN MARWANA,. ALILETA HAO WAARABU KUTOKA(SYRIA) KATIKA MWAMBAO WA PWANI. WALIJENGA KATIKA MIJI YA PATTE. LAMU.. MALINDI. KILWA. ZANZIBAR. MOMBASA. NAMIJI MINGINEYO KATIKA MWAMBAO WA PWANI YOTE YA AFRICA YAMASHARIKI.. BAADAE WALIKUJA WAARABU WENGINE WALIPOPATA KHABARI KUWA JAMAA ZAO WAMELETWA KATIKA NCHI HIZI ZA PWANI. MKUBWA WAO KATIKA HAO WALIOKUJA ALIKUWA KIITWA HAJ SAID. WALIPOKUWA WENGI HAO WAARABU KATIKA LAMU WALIFANYIZA MJI PAHALA PANAPOITWA HIDABU(MLIMA HIDABU) MLIMA HUNU NI WAMCHANGA AMBAO HATA LEO UPO HAPA LAMU.. NAUNAITWA AMA KUJULIKANA KWAJINA LA MLIMA HIDABU.. HIDAB KWA KIARABU MAANA YAKE NIPAHALA PALIPOINUKA JUU YAANI MLIMA.. WAARABU HAO WALIKUWA HAWAJUI KUWA WIYONI KUWA WATU. WIYONI IPO KIBLANI NDANI YA KISIWA CHA LAMU NA MJI WA LAMU WASASA(N.W.) OF LAMU TOWN. INASEMEKANA KUWA PIA HAO WATU WA WIYONI NI ASLI YA WAARABU WALIOTOKA YUMBWA, KATIKA HIDJAZ, SASA INAYOITWA SOUD ARABIA.. YUMBWA NI BANDARI KARIBU NA MADINA. MPAKA LEO WATU HAO KIZAZI CHAO KIPO HAPA LAMU NAWAJULIKANA KWA JINA LA WAYUMBILI AMBAO ASILIYAO NI WALE (WAYUMBUWA). WAARABU HAO WALOKUWA WAKIKAA WIYONI WAAMBIWA WALIKUWA NA NGUVU SANA, HATA WAKISIWA WA LIKUWA WAPIGANAJI WAO WALIOKUWA WAKISHIKA SILAHA NIKIASI ALFUKUMI NAMBILI 12000, AMA ZAIDI. WALE WAARABU WALIOKUWA WAKIKAA HIDABU WALIPOJUWA KUWA KUNA WATU WIYONI WALITAKA KUWATAWALA NAKUWAWEKA CHINI YAO. WAYUMBILI WALIKATAA KUTAWALIWA KABISSA.. VITA VILIANZA BAINA YAO WATU WAKAAO HIDABU NAWALE WAKAZI WA WIYONI.. WALIPIGANA SIKU NYINGI SANA, BAADAE PANDE ZOTE MBILI ZILICHOKA KUENDELEYA NA VITA WAKATAKA KUFANYA AMANI. BILA KUJUANA.. HIDABU WALIANDIKA BARUWA ILI KUWAPELEKEYA WATU WA WIYONI KAPEWA MJUMBE KWENDA NAYO.. KIFIKA NJIANI KAKUTANA NAMJUMBE WA WIYONI ENDAO HIDABU NABARUWA YAO.

ULE UJUMBE WAWIYONI KASEMA NENDAO NA BARUWA HINI KUTAKA KWENI UJUMBE WA HIDABU ALIPOSIKIYA VILE YEYE KASEMA MIMI NENDAO NA BARUWA YA UJUMBE WAKUTAKA VITA VIKALI VAMWISHO. ALIMSHINDA KWA AKILI KAMUHADAA(KAMDANGANYA). WAKAFUATANA PAMOJA WAKENDA HIDABU. KAWAELEZEYA WATU WAKE. BAADA YA KUSOMA ILE BARUWA WAWATU WA WIYONI. WATU WAHIDABU WALIJIBISHA BARUWA KALI YAKUTAKA VITA VIKALI VAMWISHO. WATU WAWIYONI WASIWEZE TENA KUPIGANA WAKAOMBA AMANI.. HIDABU ILIKUBALI KWA SHURUTI. JESHI LAWIYONI LOTE LIJE HIDABU BILA KUCHUKUWA SILAHA YOYOTE YENU. ALIKUWAKO MZEE WAWIYONI KAWAMBIYA MUSIKUBALI KWENDA BILA KUCHUKUWA SILAHA ZENU SABABU SIKU YA SULUHU (AMANI) NDIYO SIKUKUBWA YAVITA. LAKIN WALIMPUZA MANENO YAKE KWAKUMUONA ATI MEPISWA HANA AKILI TENA KWA UZEE. WALIKWENDA BILA KUCHUKUWA SILAHA ZAO.. WATU WAHIDABU WALIWASHAMBULIYA KWA MAJAMBIYA NAKUWAUWA WAKAWAANGAMIZA KABISA MPAKA WASIWEPO TENA WATU WAKUWEZA KUPIGANA.. IKAWA NDIYO SABABU YAKUSHINDWA KABISA.. BAADAE WALIWATAWALA, WALIWAKATAZA KUJENGA WAJUMBA YA DARI(GHOROFA) WAKAWALAZIMISHA KUWA NIWENYE KUOSHA MAITI ZAO, WAKAWAKATAZA KUVAA VIATU.

SASA TURUDIYE KATIKA MAKABILA YA LAMU..

KAWA TULIVOSEMA ASILI YA WATU WA LAMU NIWAARABU KUTOKA(SYRIA) AU KWAJINA LINGINE DIMISHKI-ASHAM. WALIKUJA WAKTI WA EZZI YA KHALIFA WATANO WA UMMEYED(BANU UMAYYA)A.H.65-86.A.D. 685-706. WALIWAKUTA WAARABU WALE WA YUMBWA WALIOTOKA HIDJAZ SASA SOUD ARABIA. WALIKUJA NA WAARABU WENGINE MBALIMBALI AMBAO TUTATAJA KHABARI ZAO WALIKUJA WAARABU WAKASHUKIYA MOMBASA KUTOKA JIDDA(HIDJAZ) SOUD ARABIYA. WATUHAO SASA WAITWA WAJONVU.WANANCHI HAO NIKATIKA WAARABU WALIOKUJA JIMBO HILI LA PWANI MAPEMA SANA KUTOKA JIDDA WALIFIKIYA KARIBU NA KISAUNI PANAPOITWA JUNDA. WALIPOONDOKA JUNDA WALIKWENDA MVITA. SASA YAITWA MOMBASA. KATIKA HAO WALIOFIKA MAPEMA NI KHAMIS BIN HAJI AU HAMISI BIN MWINYIHAJI NAWAPILI NI MWINDADI BIN MWINYI. KADHALIK WASHIRAZI WALIKUJA KUKAA MVITA NAMKUBWA WAO WALIMWITA SHEIKH MVITA.. WATU HAO WALIENEYA NAKUTAPAKAA KUKAA MOMBASA. MALINDI. GEDE. KILIFI NA SHAKA. MTWAPA. WATAMU. AWA KABILA ZA WATU WA LAMU. ALIEKUJA KWANZA NI YULE HAJI SAIDI. NABAADAE WALIKUJA WAARABU WENGINE WALIOPITIYA INDIAN OCIAN WAKAJA NAMICHE YA MINAZI. HAWA WALIJIUNGA NAWENZAO WALIOTANGULIYA KUJA KINA HAJI SAIDI. WALITAKA KUWEKA MKUBWA WAO(CHIEF) WALIMCHEGUWA HAJI SAIDI AME MKUBWA WAO SABABU KUWA NDIE ALIEKUJA MBELE HAPA PWANI.

WALE WAARABU WALIOKUJA NAMICHE YAMINAZI WAKAPEWA JINA KINAMTE KWAVILE WALIVOLETA MICHE YAMINAZI. NAKIZAZI CHAO KIPO HATA LEO HAPA LAMU. NAKILE KIZAZI CHA HAJI SAIDI ALIEPEWA UKUBWA(UCHIEF) WA UZEE WA MJI KIKAITWA WAUNGWANA WAYUMBE. MAANA YAKE NYUMBA YA MTAWALA. HAWA PIYA KIZAZI CHAO KIPO HAPA LAMU. HATA LEO: PATTE KIPO NYUMBA INAYOITWA YUMBE KWAMWENYEMUI. MAANA YAKE DIWANI AU PALACE. INGAWA WALIKUBALIANA KUWA HAJI SAIDI AWE CHIEF AMA MZEE WAO WAMJI YAANI KAMA MTAWALA. LAKINI HAJI SAIDI ALISEMA MIMI NIMEKUBALI NIWE MKUBWA WENU WAKUKATA SHAURI LAKINI NATAKA KATIKA KILA KABILA ATAWALISHWE MTU M'MOJA KWANJIYA YAUCHEGUZI WAKILLA MWAKA UWE UCHAGUZI WAKUKUBALIANA. NAIKAWA NDIYO MWENDO WAO. HAWAKUTAWALIWA NAMTU YEYOTE. BAADAE WENYEWE WATU WA LAMU NDIYO WALIKWENDA KWA SEYYED SAID BIN SULTAN AL-BUSSAID AMBAE SASA WAJULIKANA KWA UFALME WA ALSAID KUOMBA HIMAYA.(PROTECTION) SEYYED SAID NDIE ALIEKUWA MTAWALA WA OMAN NAPWANI YOTE YA EAST AFRICA. -SABABU YA WATU WA LAMU KUTAKA KUINGIYA KATIKA HIMAYA YA SEYYED SAID MTAWALA WA OMAN TUTAITAJA BAADAE KWAKIREFU.

WALIKUJA WAARABU WENGINE AMBAO JAHAZI YAO ILIZAMA NA BAADHI YAO WAKAOKOKA(WAKASALIMIKA). WAKAPEWA JINA. WAFAMAU. MAANA YAKE WALIOKUFA MAJI. YAANI WALIOZAMA BAHARINI. HAPO JAHAZI YAO ILIPOZAMA NIKARIBU NA LAMU PANAITWA FORMOSA AU ZIWAYUU. HAWA KINAMTE NA WAFAMAU NA WAUNGWANA WAYUMBE WALITOWA KABILA ZAO AMBAZO SASA ZAJULIKANA KWAMILANGO ITHNAASHARA YA LAMU. NAWALE WATU WALOKUWA WIYONI WAKAWA WAJULIKANA KWAJINA LA WAYUMBILI. MAHATA LEO VIZAZI VOTE HIVO NILIZOZITAJA VIPO LAMU.

VITA VA WATU WA LAMU NA WA PATTE

VIPO VISIWA VITATU VIKUBWA NA VIDOGO VINGI KARIBU NA LAMU. KISIWA CHA PATTE NIKIKUBWA ZAIDI. KIPO KIBLANI MWA LAMU(N.E.) CHAPILI KWAUKUBWA NI KISIWA CHA LAMU. KIPO NAKISIWA CHA MANDA KILIOPO KARIBU NA LAMU, MASHARIKI YA LAMU NA NIKIDOGO KULIKO KISIWA CHA LAMU: PATTE NA MANDA ZILIKUWA ZIMETAWALIWA NA WAFALME WAO: PATTE WALIKUJA WAARABU ASILI ZAO WALITOKA OMAN MUSCAT KABILA YAO ILIKUWA NABAHANI. WALITAWALA PATTE WAKAWA NANGUVU SANA, BAADAE WALIMPIGA MFALME WA MANDA WAKAWASHINDA NAKUIVUNJA KABISA. WATU WA MANDA WALIKIMBILIYA LAMU. LAMU ILIWAKARIBISHA WEMA. WAKAPEWA RUHUSA WAKAE HAPA KISIWANI PAHALA PANAPOITWA SHELA WPAKA SASA KIZAZI CHA HAO WATU WA MANDA KIPO HAPA SHELLA, KISIWANI LAMU.

WA PATTE WALITAKA WAMANDA HAO WARUDISHWE PATTE. LAMU WALIKATAA KUWARUDISHA. IKAWA NDIYO SABABU YAKWANZA YA VITA.
KAMA NILIVOTANGULIYA KUSEMA WATU WA LAMU HAWAKUTAWALIWA NA MFALME YEYOTE. WALIKUWA WAKICHEGUWA MKUBWA WAO KILLA MWAKA. WAKATI PATTE ALIPOKUWA MFALME WAO AKIITWA BWANATAMU ALITAKA KUIPIGA LAMU NAKUITAWALA LAKIN WA LAMU WALIKATAA KUTAWALIWA. WA PATTE WALIJIFUNGA VITA KUJA KUIPIGA LAMU. PANA PAHALA HAPA LAMU AMBAPO NI MTO WABAHARI MWEMBAMBA SANA PANAITWA MKANDA MADAU YOTE YATOKAYO PATTE HUPITIYA MTO HUWO KUJA LAMU. WATU WA LAMU WALIUZIBA MTO HUO ILI MAJESHI YA PATTE YASIWEZE KUPITISHA MAJESHI YAO KWA URAHISI(USAHALI).. MFALME WA PATTE ALIJENGA MTEPE MKUBWA UKAKOKOTWA(UKABURUTWA) TOKEYA MAGOGONI HADI KIKONI (KIVUKONI) MOKOWE. HAPO WALIPAKIWA ASKARI NAKULETWA HADI LAMU.. KULIPIGANWA VITA VIKALI BAINA YA ASKARI WA PATTE NAWATU WA LAMU.. WAPATTE WALIPIGWA SANA NAKUULIWA.. INASEMEKANA HATA WANAWAKE WA LAMU WALIINGIYA KATIKA VITA HIVO. WAKIWAPIGA KWA MITTI ASKARI WA PATTE.. MITTI NI ILE WANAYOTUMIYA WANAWAKE KUTWANGIYA MAHINDI, MPUNGA NA VITU VINGINEVO: WAPATTE HAPO WALISHINDWA KABISA. LAMU IKAWA NANGUVU.
INASEMEKANA KUWA MANDA NI YAZAMANI SANA HATA HUSHINDA LAMU NA PATTE NANIKATIKA KILE KIMOJA CHA VISIWA VA SOFALA CHENYE BANDAR YA BIASHARA YA DHAHABU. HAPO ZAMANI WA MANDA WALIKUWA WAKIJULIKANA KWAJINA LA WAVAA N'GANDU..(WAVAA DHAHABU) NAILIKUWA NANGUVU SANA WAKATI ILIPOVUMBULIWA NA SULAIMAN BIN SULAIMANI AMBAE NDIE MTAWALA WA MWANZO WA KI NABAHANI ALIEITAWALA PATTE.
ALIFIKA PWANI YA KENYA MWAKA 1204. A.D. MFALME WA PATTE ALIKUWA MJEURI SANA , NA ALIKUWA NA NGUVU KUBWA. KABLA MANDA KUVUNJWA ALIKUWA KIWAKATAZA WATU WA MANDA WASISOWE (WASTWANGE) NAFAKA ZAO WAKATI WAMCHANA ATI YEYE HUWA AMELALA KISIWANI PATTE.. MFALME WA PATTE ALIKUWA NAMTOTO AMBAE NI JEURI SANA KIWAFANYIYA WATU UDHIYA NA JEURI KILA NAMNA.. ALIKUWAKO MZEE M'MOJA KACHOKA SIKU MOJA KAMWAMBIYA M'GU TAKUPELEKA LAMU TUKUONE HIZO JEURI ZAKO UTAFANYA NINI ULE MTOTO ALIKASIRIKA SANA. HAPOHAPO KACHUKUWA DAU LAKUVUKIYA KAVUKA KENDA LAMU. INGAWA ALIKUWA NI MTOTO WA KIFALME LAKIN ALIKUWA NI MGENI HAJUI POPOTE LAMU. KAFIKA NJE YA MJI PAHALA PENYE KIWANRA CHA WAJUME..(MAFUNDI WANAOTENGEZA PANGA) KAINGIYA MTOTO WA LAMU NA UPANGA WAKE KAUNOWA KWENYE KINOO BAADAE KIGEUKA KAMUONA MTOTO SURA ZA KIGENI, ALIKWENDA KASHIKA NGUWO ZAKE KAFUTIYA ULE UPANGA WAKE BILA KUJALI KUWA MEFANYA KITU KATOKA KENDA ZAKE. ULE MTOTO WA KI FALME KUONA VILE ALIPANDA DAU LAKE KARUDI KWAO.

akisema NJE YA MJI MAMBO NIHAYA JE KIINGIYA NDANI YA MJI WATANIFANYAJE? IKAWA NDIYO DAWA YAKE YA KILE KIBURI CHAKE ALICHOKUWANACHO NAKWATENDEYA WATU AKATUBU. KATIKA MWAKA 1330 MTAWALA WA PATTE AMBAE ALIKUWA MABAHANI MOHAMAD II WAKIMWITA BAKIUMBE AMBAE NDIYE ALIEIPIGA MANDA LAKIN HAKUISHINDA MPAKA MWAKA 1390 ILIANGUKIYA MANDA KATIKA MIKONO YA OMAR I ALIERITHI KITI CHA EZZI KUTOKA KWA MOHAMAD II NA KATIKA UTAWALA WAKE NDIYO MANDA ILIANGUKIYA MIKONONI MWA MFALME WA PATE NANDIE ALIE ISHINDA NA KUIVUNJA KABISA.
LAMU ZAMANI ILIKUWA IKIITWA KIWANDREO(KISIWA CHA KIBURI.) PATTE IKIITWA PATEYUNGA MAANA YAKE WATU WAKAOKWENDA WAKIYONGOWA NJIANI KWA KIBURI NA MAJIVUNO.

SIWA YA LAMU YA SHABA NA SIWA YA PATTE YA PEMBE.

TULIPOKEYA KWA WAZEE WANAOSEMA KUWA SIWA YA LAMU YA SHABA ASILI YAKE YATOKA PAHALA PANAITWA KINARANI KARIBU NA KITAU KISIWANI MANDA. WALIKWENDA WATU WA LAMU WAKAWAPIGA VITA WAKAWASHINDA LAKIN BAADA YA KHASARA KUBWA ZA ROHO ZAWATU WA LAMU NYINGI KUPOTEYA. WALIIPATA HIYO SIWA YA SHABA NA ZINGAMII ILIOKUWA MFANO WA SIWA LAKIN ILIKUWA KUBWA KULIKO SIWA ZAID SANA NA NZITO, WASIWEZE KUICHUKUWA WAKAITOSA BAHARINI. NAHINI SIWA PIYA ILIKUWA NA KIPANDE CHA JUU KIZITO SANA AMBACHO WALIKIPUNGUZA WAKAKITOSA BAHARINI NAIKABAKI HINI ILIOKO SASA. ILIPOKUWA THAMANI YAKE NI ROHO ZAWATOTO WAO WENGI WALIOPOTEZA NA MAISHA YAO, ILIWEKWA WAKFU KWAVIZAZI NAVIZAZI MPAKA MWISHO WADUNIYA IWE NIUKUMBUSHO WAO NAKUWA ITUMIKE KATIKA JAMBO KUBWA KAMA ARUSI YAWENYE ASILI YAWALE TULIO TANGULIYA KUWATAJA MAKABILA YAO KATIKA YALE MAPOTE AMA MILANGO ITHINAASHARA YA ASILI YA LAMU WALIOPOTEZA ROHO ZAO MPAKA KUIPATA ILE SIWA YA SHABA.
AMA ILE SIWA NYINGINE YAPEMBE YA PATE AMBAYO ASILIYAKE YATOKA PATTE, HAPA PANA CHAWANYO KIKUBWA. PANA WATU AMBAO HAKI YAO NIKUPIGIWA ILE SIWA YA LAMU TU KWASABABU NIKIZAZI CHA WALE WATU WALIOPOTEZA MAISHA YAO KWA AJILI YAKUIPATA ILE SIWA YA LAMU IPO SIWA NYINGINE YAPEMBE YA PATTE. WALE WATU WA LAMU WASIOZALIKA NAWATU WA PATTE HAKI YAO NIILE SIWA YA LAMU TU WATU WALIO ZALIWA NA WA LAMU LAKIN WAMECHANGANYA KIZAZI NA WA PATTE HAO WANAHAKI YAKUPIGIWA SIWA ZOTE MBILI YA LAMU NA YA PATTE.
WAKO NAWATU WENGINE AMBAO HAKI YAO NIKUPIGIWA SIWA YA PATTE TU KWAKUWA NI WAARABU WAGENI WALIOINGIYA BAADA YA KUFANYIZWA, MIPANGO YA MATUMIZI YA SIWA YA LAMU, NA SIKIZAZI CHAWALE WAASILI YAWALIOPIGANA KINARANI KWA AJILI KUIPATA ILE SIWA YASHABA

inavofikiriwa nikuwa SIWA ZOTE MBILI ZINA ASILI ZA KI SHIRAZI AMBAO WALIISHI ZAMANI KATIKA MWAMBAO WAPWANI HINI YA KENYA SABABU MAANDISHI YAKE YALIOMO KATIKA SIWA ZOTE MBILI NI YA KISHIRAZI. BAADHI YAWATU WASEMA HIVI:- ATI SIWA YA LAMU ASILI YAKE WATOKA MUDIYO(HIDIYO) HIYO HIDIYO IPO BARA MAGHARIBI YA MKUNUMBI, LAKIN HILO HALINA MSINGI MWEMA WAKUWEZA KUTEGEMEWA SABABU WOTE WALIOKUJA MWANZO WALISHUKIYA UPANDE WA KITAU NA TAKWA NA SHAKA AMBAKO ALAMA ZA MAJENGO YAO HATA LEO ZIPO ZAONEKANA WALIZOJENGA ZAMANI. HUKO MUDIYO AU HIDIYO HAKUNA ALAMA YOYOTE YAMAJENGO WALA NYINGINE. KITAU INASEMEKANA KUWA NDIYO NCHI AU RASI YA MWANZO ILIOONEKANA NA WALE WAFUASI WA ABDULMALIK BIN MARWANA KHALIFA WATANO WAKINA BANU UMEYYA. KITAU IPO (S.W.) POINT YA MANDA IMEKABILIYANA NA SHELLA ILIOKO KISIWANI LAMU. INAAMBIWA KUWA MTAWALA WAKE ALIKUWA MWANAMKE KIITWA MWANA. MPAKA LEO KISIWANI MANDA PANA PAHALA PANAITWA RASIYAMWANA. HUYU MWANAMKE MWANA INASADIKIWA KUWA ALIJITOSA BAHARINI NA KUFA AMA ALIJINYONGA WAKATI ALIPOSIKIYA WAZEE WA MJI WAKE WAMEJITIYA KATIKA TWAA AMA HIMAYA KWA MFALME WA PATTE ALIEKUWA KIITWA FUMO OMAR WAKIZAZI CHA NABAHANI. LAKIN WATU WENGINE WASEMA ALIKWENDA KUISHI PATTE MPAKA KUFA.

SASA TUTAENDELEYA NA KHABARI YA VITA.

WATU WA PATTE WALIAZIMIYA KUJA TENA KUWAPIGA WATU WA LAMU. WALIPOSIKIYA WATU WA LAMU NDIYO WAKAFANYIZA MPANGO KUCHUKUWA HIMAYA KWA LIWALI WA KI MAZRUIY AMBAE ALIKUWA METOKA TWAANI KWA SULTANI WA OMAN(REBEL) AMEFANYA MOMBASA MAKAO YAKE.(ASIMA) LAMU HAPO KULIKUWA NA PART MBILI. MOJA IKIITWA SOUD. NAMOJA IKIITWA ZENA. MTAWALA WA SIKU HIZO (RAIS) MTEULE ALIKUWA NI BWANA ZAHIDI MG'UMI BANUMAKHZUMIY. YEYE HAKUPENDELEYA SHAURI HILO.. LAKIN IKAWA IFANYWE VOTE YAKINA SOUD WATAKAO WAKASHINDA WALICHUKUWA HIMAYA KWA LIWALI WA MOMBASA. ALIKUJA LIWALI ABDULLA BIN HEMED MAZRUIY KWA JAHAZI YAKE NA ASKARI WAKE LAMU WAKATI HUO WENYEWE WATU WA LAMU WALIKUWA WAKIJENGA NGOME. MCHANA ULE LIWALI ALIKUWA KISHUKA MJINI KUKUTANA NA WAZEE KULE NGOMENI, NAJIONI KIRUDI JAHAZINI MWAKE CHENDA KULALA. BWANA ZAHIDI BILA KUTAJA KWA MTU YEYOTE ALIANDIKA BARUWA KAFANYA NAZAWADI KAMPA MTUMWA WAKE ANAEMUAMINI SANA KAMWAMBIYA USIKU WAMANANE CHUKUWA DAU UJIFANYIZE KUWA WATOKA PATTE WENDE JAHAZINI KWA YULE LIWALI UMPE BARUWA HINI NA ZAWADI UMWAMBIYE ZATOKA KWA MFALME WA PATTE UPOKEE NA MAJIBU UJE NAYO BILA KUJUWA MTU YEYOTE

MTUMISHI YULE KAFANYIZA KAMA ALIVOAMRIWA NABWANAWAKE KENDA NA KARUDI NA JAWABU. BWANA ZAHIDI ALIKUWA AMEWTANDIKIYA HIVI:- VIPI ULIMIAHIDI KUWA UTAMITILIYA MIKONONI LAMU, MPAKA LEO BADO HUJAFANYA CHOCHOTE? SULTANI WA PATTE..

ULE LIWALI WA MOMBASA ALIJIBISHA BARUWA KWA KUSEMA:-
AHADI YANGU NI ILE ILE, LAKIN SIJAPATA MAKUBADHI SAWASAWA YAANI WASHIKO MADHBUTI, WANGOJEYA NGOME IKISHA KUKAMILIKA KUJENGWA NDIYO NITEREMSHE ASKARI WASHIKE NGOME NAKUSHIKA MJI WOTE, HAPO NDIPO NITAKAPO KUKUPA KWAMKONO. ABDULLA BIN HEMED MAZRUIY.

ASUBUHI MAPEMA BWANA ZAHIDI ALIITA MKUTANO WAWATU WOTE NDANI YA NGOME NAKAWAMBIYA KILLA ANAEKUJA AJE NASILAHA ZAKE ZAVITA KAMIL WATU WOTE WALIFIKA PAMOJA NA SILAHA ZAO KAMA WALIVOAMRIWA. SAA4 ULE LIWALI KAMA ADA YAKE ALITEREMKA KUTOKA JAHAZINI MWAKE KENDA NGOMENI.. ALIONA UKUTA WAJENGO UMESONGWA KWA JENGO NAKUBAKISHWA NJIYA NYEMBAMBA YAMEANGO TU NAWATU WAMEJAA PAMOJA NASILAHA ZAO KAMIL ZAVITA. BWANA ZAHIDI ALIITOWA ILE BARUWA YAYULE LIWALI KAWASOMEYA WATU,. NAKAMUULIZA YULE LIWALI WAKI MAZRUIY BARUWA HIN? NIYAKO? KAJIBISHA NAAM NIYANGU: KAMWAMBIYA TULIKWITA SISI WENYEWE, NASASA KUKUUWA KWETU NIAIBU. WAUNGWANA HAWASHIKWI KWA HILA. TOKA WENDEZAKO. NAKAMA NISHUJAA KWELI KAJIFUNGE TUPAMBANE KWAVITA TUKUSHINDE AMA UTUSHINDE. ABDULLA BIN HEMED MAZRUIY HAPO BADALA YA KWENDA ZAKE MOMBASA ALIPOTOKA LAMU ALIKWENDA PATTE WAKAFUNGA VITA PAMOJA NA MFALME WA PATTE KUJA KUIPIGA NAKUSHAMBULIA LAMU KWA NGUVU KUBWA..

SASA TUTARUDIYA NYUMA KIDOGO

ZAMANI WATU WA LAMU BAADA KUWASHINDA WATU WA KITAU KINARANI NA PATTE NA PIA WATU WA MVITA KABLA MAZRUIY KUISHIKA MOMBASA WATU WA LAMU WALITAKA KUJILIPIZA KISASI KWA WATU WA MVITA AMBAO KILLA MARA WALIKISEMA WATU WA LAMU SIWAPIGANAJI KAZI YAO NISTAREHE NAKULA KONDOO WATU WA LAMU WALIJIFUNGA KWENDA KUWAPIGA VITA KWASABABU YAMANENO YAO HAYO. LAKIN WAKIFIKA KILIFI UPEPO WAKUSI ULIKUWA MKALI NA MIVUA MINGI. WATU WA LAMU HAWAKUWEZA KUFIKA MOMBASA WALIRUDI KWAO.. WATU WA MVITA WALIPOPATA KHABARI KUWA WATU WA LAMU WAMERUDI WALITUNGA NYIMBO WAKASEMA:-

(1) muliokoma kilifi, musiweze vuka vuma:
kwakucha wavuwa chafi, kiroboto namanyema:
mukishindiya ulafi, kwandamana nyuma nyuma :
kuziwitiyya hishima, mapepe mutiziyeni:

(2) hoko sikusitarehe, kwakondoo na mibuzi:
wakucheka he-he-he-he, vicheko va udekuzi
kuwaoneya mahehe, mukiwa henda pumzi:
mewgine hamuyawezi, kwamba mwaweza njooni.

HAWA KIROBOTO NA MANYEMA WALIKUWA NIWATUMWA WA MAZRUIY WALIOKUWA WAKIKAA TAKAUNGU KAZI ZAO WALIKUWA NIWAVUVI WASAWAKI. NYIMBO HIZI ZINAONESHA KUWA WATU WA LAMU HAWAKUWA NIWATU WAVITA. BALI KAZI YAO NI STAREHE KULA MANYAMA WAKWENDA WAKITOWA PUMZI WAKUYONGOWA VITA HAWAZIWEZI: BAADA YA MVUWA NAUPEPO MKALI KWISHA WATU WA LAMU WALIKWENDA KUSHAMBULIYA MOMBASA WAKUVUNJA MJI WAKALE. BAADAE WATU WA PATTE NA MOMBASA TENA WALIFANYA MPANGO KUJA KUISHAMBULIYA LAMU. SABABU ILIKUWA KAMA IFUATAVO:- YAAMBIWA KUWA MFALME WA PATTE BWANA BAKARI WABWANAMKUU ALIOWA MWANAMKE WA LAMU AKAZAA WATOTO WAWILI WANAWAKE KAWACHUKUWA PATTE KATIKA BANATI HAO M'MOJA ALIOLEWA NA BAYAYE WASHIYE, KAMZAA FUMO LUTI. WAKTIHUO MFALME ALIKUWA BWANA MADI, AKAUSIYA AKIFA UFALME APEWE FUMO LUTI WABAYAYE, SABABU YA KUPATA NGUVU NAUMOJA WAWATU WA LAMU KWAAJILI YA YULE MTOTO WAO ALIEZALIWA. WATU WA PATTE WALIKATAA WAKAANZA KUPIGANA WAO KWAWAO. WATU WA LAMU WALIKWENDA KUSAIDIYA UPANDE WAMTOTO WAO. VITA VILIENDELEYA SIKU NYINGI NAIKAWA NDIYO MWANZO NAMSIGI WAFITINA KHASA BAINA YAWATU WA LAMU NA WAPATTE. BWANA BAKARI WA BWANAMKUU ALIKUFA MWAKA 1768, BAYAYE WASHIYE YASEMEKANA KUWA [illegible] NIKIZAZI CHA BAYAYE BIN MKUU JAMALILLEIL AMBAE NDIYE ALIEITENGENEZA ILE SIWA YA PATTE KUMTENGENEZEYA MWANADARINI KATIKA MWAKA 1698. BWANAFUMO MADI ALIKUFA KIASI MWAKA 1809. AHMAD SHEIKH ALITAWALA PAHALA PA BWANAMADI KWAMSAADA WA MAZRUIY WA MOMBASA. WALIKUJA KUISHAMBULIYA LAMU LAKIN WALIPIGWA SANA. WA MOMBASA KAKAKIMBIYA. BAADA KUSHINDWA VITA HIVO MWAKA 1812 NAYULE LIWALI MAZRUIY KUTOKA NAKWENDA PATTE WALIJIFUNGA VITA KWAKUSHIRIKIYANA WA PATTE NA WA MOMBASA KUJA KUISHAMBULIYA LAMU KWANGUVU KUBWA. HIZI NDIZO NYIMBO WALIOKUWA WAKIJIBIZANA BAINA YAWATU WA LAMU, NA WAPATTE, NA WA MOMBASA KABLA YA VITA KUANZA. KAMA NILIVOTANGULIYA KUSEMA LAMU KULIKUWA NA PART MBILI. CHAMA KIMOJA KILICHOMTAKA ULE LIWALI WA MOMBASA WA KI MAZRUIY AWAPE HIMAYA KABLA YAKUJUWA KUWA YULE LIWALI YUPO PAMOJA NA SULTANI WA PATTE. PART ILE ILIKUWA IKIITWA SOUD. PART YA ZENA ILITUNGA NYIMBO KUTIANA HAMASA(ARI) WENYEWE KWAWENYEWE ILI WASIKUBALI KUTAWALIWA NA MFALME WA PATTE WALA MTU MWINGINE YEYOTE.

(1) Zeze na Ashahamadi, wakhubirini malenga
Ajae napige hodi, miTango tumeifunga
tumekomeya na midi, namagogo yakupinga
Kupa hirimu kutanga, kujuwa kilichondani

(2) Tatasa pato upambe, Tatanisha zibodoo
Uivumize muyumbe, siwa yetu ya mnreo
Nayandamane napembe, mishindo iwe tandao
Tukumbuke yaoitayo, igeukavo duniya.

(3) Yamshabaka furungu, Uvumizapo muyumbe
kusi zenu matawangu, nazandamane na pembe
Tukeshe yote makungu, kula mwene lake ambe
Maneno tusiyafumbe, wa'au tusiyakhini.

(4) Tukumbuke ulimwengu, Igeukavo duniya
Kizazi namoya fungu, kupinduliana niya.
Huzengel'eyana pingu, Il'imwende kumtiya.
Kilamtu chamba haya, Achambiwa aneneni?

(5) Kipilipili waume, Takukukuta kisiki
Takanami twandamane, Kwaufal'ume wa nyuki (KWAUHADIMU)
Pingani zisitwegeme, Kwamiyomo yabunduki WANYUKI..
Tufil'iye yetu haki, Tusiweke cheo duni.

(6) Kul'a mwenye mbovu niya, Bbovu dhamirini nasi
Rabbi tatuhukumiya, Tukuze zetu nafusi
Kwa auni ya Jaliya, Al'iye Mola mkwasi
Kufuata mfuasi, Hilo hal'ipatikani.

(7) Mla shokowa la pemba, Nakwetu ataka kul'a.
Meifanya kuwa simba, Kuya pasina muhula
Uyao kiwamba wamba, Nakutwegesha madhila.
Akiya tashuka shela, Soudi mutatendani?

(8) Pani shauri Soudi, Nil'iyuwe namapema
Ambal'o l'enye muradi, Kwani muwana wazima
Isiwe kutaradadi, Iyapo siku yakwima
Tufe katika hishima, Tusiweke cheo duni.

JAWABU LA KINA SOUD WALISEMA

(I) Lakutenda situuze, Situuze l'akutenda
Metufunda mwanamize, Mwanamize meufunda
Kuwapunda tuizize, Tuizize kuwa punda
Kwandikwa tapo tuchenda, Hilo hal'ipatikani

(2)
Ufe liwali wa KI MZRUIY ABDULLA BIN HAMED ALIKIWAITA WATU WA LAMU MAJIMBI(MAJOGOO) WANAORANDA UWANJANI, KITOKEYA JOGOO MKALI WAO HUJIFICHA HAWAWEZI KUPIGANA VITA, LAO NIMANENO TU, NAKUSTAREHE. KWAHIVO WAKUBALI WAJIZUNGUMZE NAWAINGIYE TWAANI YAANI WAJITOLEE AU (SURENDER) KWAMAJESHI YA WAPATE NA MOMBASA LAMU WALIKATAA KABISA NA WALIWAPELEKEYA NYIMBO HIZI:-

(I) Hela tunda kwa dal'ili, Kwamba wataka maana
Jimbi mtambiya mbal'i, Mtasamba na kudona
Huuzwa tye makali, Kiwandani akiwana
Tusiye onana yana, Nayeo hatuonani.

(2) Twaapa kwa Mol'a awga, Dhul'i sizenye tupata
Nasi tul'ina mizinga, Ambayo tutakukuta
Soudi wal'ina panga, Wataye wenye kuzita
Turadhi sambe kutota Sute tukawa maini.

(3) Tuketiziye tayari, Watumwa kwa waungwana
Mkunduki mshamari, Tukatuziye na tana
Ili kuziwiya ari, Wazelle wetu na wana
Kwamahadazi hapana, Wal'ipitil'e zamani.

(4) Inshaal'ah tumo jahani Kanakwamba kiwanreo
Muyatakapo mawani, Nutafidi muradiyo
Hatutiwi khafukani, Nakufishwa zetu nyoyo
Nileo siku nileo, Maisha wikaburini.

(5) Twalipopija kimondo — pepe zikaneya yango
Ili kubashiri kondo, — Khasa kwanti zayunga
Kutakithiri zitendo — Nakushitadi upanga
Pepo zikisa kuzinga, — Pwani mkunguwi pwani.

JAWABU YA YULE ABDULLA BIN HEMED MAZRUIY.

(I) Mimi niko pate yunga, — Nifuete ahamadi
Kati simwenye kuzinga, — Ulimi wangu sirudi
Pinga zenu mungapinga, — Hazitengui ahadi
Siku yathuluthi hadi, — Tutaonana fundoni.
(2) Watumba musiwe kole, — Mukakaa kando kando
Vutikani muje mbele, — Tuoneshane vitendo
Mutaona wateule, — Wafundiye nguwo pindo
Siku yakutinda fundo, — Tutaonana fundoni.

JAWABU YA WATU WA LAMU.

(I) Muhibu wangu mgwana, — Nione wako waraka
Kifahamiya maana, — ~~[illegible]~~ kiteko kilinitoka
Nguwo muyapofungana, — Zitawakusa mashaka
Mtoteya zisokaka, — Mesiri kuwa kizani.
(2) Kwamba uko pape yunga — Nami niko Kiwandreo
Sikae ukijipanga, — Hufidishi muradio
Mume huja akasonga, — Hasemi leo ni leo
Uole mbwawa walio, — Watendavo msituni.
(3) Rijali kukaa kando, — Tuna hoja shariiya
Ule mtamani kondo, — Ndiye mwenye kurubiya
Maneno yaso kitendo, — Mwishowe Hujinamiya
Jaribu kutegemeya, — Tukutaneni fundoni.
(4) Simba kiwa maindoni, — Hufinika zake ndole
Huzivika mchangani, — Muindwa asiziole
Uliza utasakani, — Ujinga uzingatile
Nyoka za ng'OngO kubele, — Hatuchi situtisheni.
(5) Hatuchi situtisheni, — Hatuituki mishindo
Tangu kale nazamani, — Niwazowevu wa kondo
Jivu Pamoto wakuni, — Tutaliitenda vitendo
Siku yakutinda fundo, — Tutaonana fundoni.
(6) Wallahi naapa kwa Mg'u, — Na Mtumi Mohamadi
Ndoni munywe matungu, — Mubadilike jasadi
Muwe karamu ya Tungu, — Natai kuwafisidi
Natamaa yakurudi, — Kwenu musifikirini.
(7) Mukiwa miwenye kuya, — Pasiwe na mshawasha
Kwanza fanyawi wasiya, — Yawana kuwarithisha
Wake muwape zifaya, — Maeda yao kwewsha
Mukiya tutawashusha, — Mashukiyo yazamani.
(8) Kutapongiya kondoni — Nasi hapa huwalinda
Nguwo zenu zifungeni, — Mwambiye makhodha ponda
Tuketiye milangoni, — Hutunda lakuwatenda
Mwisapo pata mkanda, — Nasi tushukiye pwani.

HAPO WATU WA PATTE NA YULE LIWALI WAKI MAZRUIY WALILETA JESHI LAO KUBWA PAMOJA NAWANYIKA(WAGIRIAMA) SILAHA ZAO ZILIKUWA BUNDUKI ZA KUSHAMIRI KWA BARUTI, NA ZEMBE(MISHARE). HAWAKUPITA KWANJIA YA MKANDA BALI LILISHUKA JESHI LAO KWA UPANDE WA SHELLA. KAMA ISEMEKAVO ALIKUWAKO SHARIFF MWANA CHUONI(ALIM) MKUBWA KIITWA ABDUSWAMAD WALIMWENDEYA KUTAKA SHAURI

KAWAMBIYA NILETEENI WATOTO WATATU WASIOBALIGH WAJITOLEE KUFA KUPONA (COMMANDOS) KAPELEKEWA KAWAANDIKA DUA KATIKA MIKONO YAO M'MOJA KAMPA YAI NA UTASA, WAPILI KAMPA BENDERA, WATATU KAMPA KONDOO. KAWAMBIYA ENENDANI HATA PENYE MAJESHI YA ADUI MBELE YAO, MWENYE YAI ALIRUSHE JUU NA ALIKINGE KWA ULE UTASA AUWIKIZE ULE UTASA PAMOJA NA LILE YAI LILILOVUNDIKA AGEUKE AKIMBIYE BILA KUTIZAMA NYUMA HATA KAMA TAPIGWA RISASI. ULE MWENYE KONDOO AMCHINJE KONDOO AGEUKE AKIMBIYE ASITAZAME NYUMA, MWENYE BENDERA AICHOMEKE ILE BENDERA YAKE KWENYE DAMU YA KONDOO AGEUKE AKIMBIYE ASITAZAME NYUMA HATA KAMA WOTE WATAULIWA KWA BUNDUKI. WALIFANYIZA KAMA WALIVO AMRIWA. MARA TU ILINYESHA MVUWA KUBWA SANA. BARUTI NA BUNDUKI ZILIROWA MAJI. PINDE ZA ZEMBE(MISHARE) PIYA ZILIROWA KWA MVUWA. ZIKAWA BUNDUKI NA ZEMBE ZAO HAZIFANYI KAZI. MAJESHI YA ADUI YALIFIKA MPAKA MLIMA HIDABU. MAJESHI YA SOUDI NA YA ZENA KWA PAMOJA WALIWASHAMBULIYA MAADUI ZAO KWA PANGA, MIKUKI, VISU NA HATTA KWA MASHOKA PIYA. MAADUI WENGI WALIULIWA NA KUKIMBIYA. ULE LIWALI WAKI MAZRUIY ABDULLA BIN HEMED NA BAADHI YA WATU WAKE KIDOGO WALIOBAKIYA WALIKIMBIYA NAKUPANDA JAHAZI LAKE KARUDI KWAO MOMBASA. WANYIKA WENGI WALIULIWA WENGINE WAKAJITOSA BAHARINI NAKUTEKWA. WALIKUWA WAKISEMA:- MJOMBA SINIURAGE KULIMA NAMANYA. MANENO HAYO WALOKISEMA HAO WANYIKA YALIKUWA MAARUFU SANA HAPA LAMU. WATU WAKIIMBA KATIKA MICHEZO YAO YA CHAMA NA NDONGE AMBAO NIMICHEZO MAARUFU HAPA LAMU TAFSIRI YA MANENO HAYO WALOKUWA WAKISEMA WANYIKA NI BWANA SINIUWE TAKULIWIYA AU BWANA MIMI NAJUWA KULIMA TAKULIMIYA.

ALIKUWAKO BWANA M'MOJA WAKI MOMBASA ALIKUWA AKIJA SANA HAPA LAMU KWA RAFIKI YAKE, MARANYINGI ALIKIJISIFU KUWA YEYE WALI KIDOGO KIKOMBENI HUSHIBA LAKIN VITA HASHIBI. SIKU HIYO ALIKUWAMO KATIKA VITA. WALIPOSHINDWA NAYEYE KWA MDANGANO WAKUSHINDWA ALIJITOSA BAHARINI. KWABAHATI NZURI ULE RAFIKI YAKE ALIMUONA KIJITOSA KAMWAMBIYA GEUKA UPIGANE VITA, VIPI WAJITOSA? SIWEWE ULIEKUWA UKISEMA WALI KIDOGO KIKOMBENI HUSHIBA LAKIN VITA HUSHIBI. AKAMJIBU BWANA TWASIMANGIZANA LEO SIKU YA INKISARI?(KUVUNDIKIWA) KAMWAMBIYA BASI TOKA UMO KATIKA DHAMANA YANGU(PROTACTION) ALIMUWEKA KWAKE BILA KUDHURIWA NA MTU YEYOTE KWA USALAMA. BAADAE KAMPA DAU PAMOJA NAWATUMWA WAKAMPELEKA MPAKA KILIFI BILA KUDHURIWA NA YOYOTE.

HIVI NDIZO VITA VIKUBWA NA ZAWISHO WALIVOPIGANA WATU WA LAMU KUPIGANA NAWATU WA PATTE WALIOUNGANA NA MAZRUI WA MOMBASA. LAMU ILIPATA USHINDI MKUBWA. KAMA NILIVOSEMA KUWA SIKU ZILE HAWA MAZRUIY WALIKUWA WAMETOKA TWAANI KWA SEYYED SAID BIN SULTANI NAWAMEFANYIZA MOMBASA KUWA NDIYO ASWIMA YAO(HEADQUARTER) WAMEISHIKA NA PEMBA NAKUTAKA KUISHIKA PWANI YOTE. UNGUJA(ZANZIBAR) ILIBAKI KATIKA MIKONO YA SEYYED SAID BIN SULTAN.

SIKU ZILE SEYYED SAID ALIKUWA KIISHI MUSCAT OMAN KWENYE ASWIMA YAKE(HEADQUARTER) AFRICA ALIKIJA LABDA MWAKAMARAMOJA AMA ITOKEE JAMBO LADHARURA AKIJA ZANZIBAR KABLA HAJAIFANYA UNGUJA KUWA ASWIMA YAKE YA EAST AFRICA(AFRIKA YA MASHARIKI).

LAMU KUCHUKUWA HIMAYA KWA SEYYED SAID AL-SAID WA OMAN

WATU WA LAMU WALIPATA KHABARI KUWA SEYYED SAID MEKUJA UNGUJA. KULIKUWA NI SIKU ZA KUSI MAJAHAZI HAYAWEZI KWENDA. LAKIN KWABIDII ZAO WALIKWENDA KWA DAU HADI UNGUJA KWAMAKASIYA(KAFE) WALIMTAKA SEYYED SAID WAKAMUOMBA AWAPE HIMAYA. SEYYED SAID ALIKUBALI LAKIN KWASHURUTI, KAWAMBIYA MWAKA HUNU SITOWEZA KUWASAIDIYA SABABU NIMO KATIKA VITA UPANDE WA BANDAR ABBAS. NAWEZA KUWAPA ASKAR KIASI 400-500 LAKIN MSHAHARA WAO MUDA WAMWAKA M'MOJA UTOKE KWENU WATU WA LAMU WALIKUBALI. WALILETEWA ASKAR WA OMAN NA HADHRAMIY KIASI 500. ~~WAMEKUWA NAO~~ WATU WA LAMU WALIKAA NAO VIZURI SANA ASKARI HAO. BAADA YA ULE MSHAHARA WALIO KUBALIANA WALIWAPA NA CHAKULA PIA. BAADA YA MWAKA SEYYED SAID ALIKUJA LAMU ALIWAULIZA ASKARI, VIPI MULIVOKAA NAWATU WA LAMU? WALIMWAMBIYA LABDA HATA WENE USINGELIWEZA KUTUTENDEYA IHSANI WALIO TUFANYIYA WATU WA LAMU. NA KWA WEMA WALIVOKAA NASI.

SEYYED SAID ALIFURAHI SANA KUSIKIYA MANENO HAYO. KAANZA KUWAPA HIMAYA NAKULETA LIWALI WAWE NAPIYA KUANDIKIYANA MIKATABA YA HIMAYA BAADAE ZILIKUJA KABILA MBALIMBALI ZA KI OMAN NA ZA HADHRAMIY. WATU HAO WALIOWANA NA KUZALIANA NA WATU WA LAMU NAMPAKA SASA ZIPO KABILA KADHA WAKADHA WAKIZAZI CHAWATU HAO.

BAADA YAHAO MAZRUIY KUVUNJWA DOLA YAO NAPIA WA PATTE WAKATI WA EZZI YA SEYYED MAJID WATU HAO WALIENEYA NAKUCHANGANYIKA SANA KATIKA MWAMBAO WA PWANI WOTE KWAKUOWANA NAPIYA UPANDE WA TANGANYIKA SASA INAITWA TANZANIA. ZANZIBAR HATTA KONGO.

LAMU HAIYAWAHI HATA MARAMOJA KUTAWALIWA NA MFALME YEYOTE, LABDA WAKATI PURTUGES ALIPOKUWA METAWALI DUNIYA NZIMA AU AFRICA YOTE KWAMUJIB WA TAREKH YAKE YAKWELI. HIZO TAREKH ZISIZOKUWA NAUSHAHIDI WOWOTE ZISEMAZO ATI PATTE ILITAWALI LAMU SIZAKWELI WALA MUSIZISADIK WALA KUZIAMINI.

HAIKUTAWALIWA LAMU MPAKA WENYEWE WALIPOJITIYA KATIKA HIMAYA YA SEYYED SAID BIN SULTANI MTAWALA WA OMAN NA ZANZIBAR NAPWANI YOTE YA EAST AFRICA(PWANI YA AFRICA YA MASHARIKI) ALIPOKUJA MWINGEREZA HAIKUWA COLONY YA UNGEREZA BALI ILIKUWA KATIKA HIMAYA YA UNGEREZA NAIKIITWA PROTECTORATE OF KENYA. SIKU ZOTE BENDERA YA SEYYED MTAWALA WA ZANZIBAR IKIPEPEYA JUU YA MLINGOTI ULIOWEKWA JUU YA ARDHI, BENDERA YA KINGEREZA IKIPEPEYA JUU YA MAJENGO YA MA OFFICER WA KINGEREZA KWAKUWA SI COLONY YAO. KENYA BARA NDIYO ILIOKUWA COLONY YA KINGEREZA NA BENDERA YAO MLINGOTI UKIWEKWA JUU YA ARDHI..

WAKATI WA UHURU WA KENYA SEYYED JAMSHID ALIYEKUWA MFALME WAMWISHO WA ZANZIBAR ALIMPA MZEE KENYATTA RAIS WAKWANZA WA KENYA MWAMBAO WAPWANI WOTE WA KENYA PAMOJA NA LAMU. SASA IMO KATIKA KENYA MOJA.

MAKABILA YA LAMU

BAADA YA KUTOKEYA HUO MCHANGANYIKO WAHAO WAARABU KUOWANA WALIWEKA MAKABILA MATATU MAKUBWA NAKILA KABILA MOJA KATIKA HIZO WAKAWA NATANZU N'NE KWAMAJINA YA KISWAHILI IKAWA JUMLA MILANGO K#####B KUMINAMBILI..

I KINAMTE HAWA WANA MAFUNGU MANE.

A.. BA MAALIM.. MA ALHUSAIN WATOKANA NAKIZAZI HIKO. WALIWEKA WAZEE WAO, NAKATIKA HAO WAZEE NI SHEE SWALEH BIN ABDULRAHMAN ALHUSAINY.NDIE WALIEMUWEKA.

B. BWANA MBEKEYA. MAHDALI WAMO KATIKA KIZAZI HIKO. WALIWEKA WAZEE WAO. KATIKA HAO WAZEE WAO ALIKUWA SHARIFF ABDULLA ZUBAIR AL AHDALIY.

C. BWANA MWENYEMUI BANU MAKHZUMI NIKATIKA WATOKANAO NAKIZAZI HIKO. NIULE BWANZAHIDI M'GUMI ULE ALIWEKWA KUWA MZEE WAMAISHA ALIPOKUFA HAWAKUWEKA TENA MZEE. KIZAZI CHAO KIPO WACHACHE MPAKA SASA.

D.. WAUNGWANA #####B. ITENAASHARA MZEE WAO ALIKUWA JAAFAR BIN ~~[illegible]~~ YUSUFF BAADA YA KUFA HAWAKUWEKA MZEE TENA.

2 WAFAMAU

A.. BWANA KHAMISI WAMWENYE MUI

HAWA KIZAZI CHAO KILIKATIKA WALA HAWAKUWEKA MZEE WAO WALIBAKI WATU WAWILI TU.

B. BWANTUMANI ALI. HAWA NIKATIKA MADDI OMAR. WALIWEKA MZEE WAO KATIKA HAO WAZEE WALIOWEKA NI ABOUBAKAR MADDI. ALIPOKUFA WAKAMUWEKA ABDULLA BIN YUSUF

C. ALMAAWIY NA MAKHATIBU - WALIWEKA MZEE WAO OMAR BIN OMAR BIN ALIY, ALIPOKUFA IKAWA MGAWANYIKO MAPOTE MAWILI MAKHATIBU WAKAMUWEKA MZEE WAO ABDULLA BIN ATHMAN WASIRIDHIYANE, MAKHATIBU WAKAMUWEKA MZEE WAO SAID BIN MOHAMAD. ALMAAWIY WAKAMUWEKA MZEE WAO ABDULLA BIN ABOUBAKAR AL MAAWIY.

D.. BWANA GOGO. MZEE WAO ALIKUWA SHEIKH FAISWAL BIN ALIY. ALIPOKUFA WALIMUWEKA JAMBENI BIN ABDULLA. ALIPOKUA HAWAKUWEKA TENA MZEE.

SWAUNGWANA WA YUMBE.

A. AL BAKRIY WALIGAWANYIKA MAPOTE MAWILI. WAZEE WAO WALIKUWA (a) JAAFAR BIN ABDULLA CHEMA (b) MOHAMAD ABDULLA CHEMA.

B.. MOHAMAD BIN YUSUF. HAWA NIZAWANYO VIWILI WAZEE WAO WALIKUWA (a) ATHMAN BIN ALIY. (b) OMAR BIN ABDULRAHMANI. NDIO WAZEE WAO.. WALIPOKUFA HAWAKUWEKA TENA WAZEE..

C.. BWANA MSHUTI WAZIRI HAWA WOTE WALINAKILIKA HAKUBAKI ILA MTU M'MOJA TU WALA HAWAKUWA NA MZEE

D.. BWANA MBEKEYA WAMWENYE MUI MA JAHADHMY WALITOKA KATIKA KIZAZI HIKO. TARAFU YA WAZEE WALIKHITILAFIANA. WENGINE WALIMUWEKA MZEE WAO JAMBENI BIN MOHAMAD ALIPOKUFA WALIMUWEKA HAFIDH BIN SEIF ALJAHADHMY.

KABILA HIZO NDIZO ZILIZOKUWA NA HAKI YAKUPIGIWA ILE SIWA YA LAMU KAMA NILIVO TANGULIA KUSEMA WAKO WATU WENGINE KATIKA KABILA HIZI AMBAO WANAHAKI YAKUPIGIWA SIWA ZOTE MBILI YAANI YA LAMU NAYA PATE KWAKUWA WAMECHANGANYA DAMU KWAKUZALIWA NA WALAMU NA WA PATTE. SASA SIWA ZOTE MBILI ZIMEWEKWA KATIKA NYUMBA YA MAKUMBUSHO MUSIUM YA LAMU.

ALHAMDULILLAH MPAKA HAPA KWAUFUPI NDIYO TAREKH YA LAMU. NAMSHUKU MWENYE EZZIMGU KUNIWEZESHA NAKUNIPA UMRI NA TAUFIK KUYANDIKA TAREKH HINI MPAKA KUIMALIZA KAMA NILIVOKUWA NIMEKUSUDIYA ILI IWE MIUKUMBUSHO KWA VIZAZI NA VIZAZI VA WATU WA LAMU KHASA NAPIYA WATU WENGINE WOTE WATAKAO KUJUWA TAREKH YA LAMU NA WATU WAKE

ntna hakika KILA ATAKAE ISOMA TAREKH HIN ATAFAHAMU UKWELI UPO WAPI. AMBAO USHAHIDI WAKE NIMEUWEKA WAZI KWAMIFANO NA MASHAIRI YA FAKE YALIOMO. MIMI NI BINADAM NAWEZA KUKOSEYA AU KUSAHAU, KWAHIVO NAWAOMBA WATU WENYE KUSOMA WAKIONA KOSA KATIKA MAANDISHI AMA MATAMSHI WAZINGATIYE ZAIDI KWAKUWA SANA NIMETUMIYA LUGHA YA LAMU. KATIKA MASHAIRI YA WATU WA LAMU.. PATE. MOMBASA WAMETUMIYA KISWAHILI CHAO WALICHOKUWA WAKITUMIYA ZAMANI HIZO KWA MAFUMBO AMBACHO SASA HUWEZI KUFAHAMU MPAKA UFASIRIWE.

SIWEZI KUTOWA AHADI KUWA TAELEZA AU KUFASIRI KWA KISWAHILI TUNACHOTUMIYA SASA LAKIN MOLA AKIPENDA KIPATA NAFASI NA UMRI UKIWEPO TAELEZA TAFSIRI ZAKE.

ALHAMDULILLAH ALAA NEEMATUL ISLAMI. WASWALLA ALLAHU ALAA SEYYEDINA MOHAMAD KHERI KHALKIHI WANURI ARSHIHI WAALAA ALIHI WA AS-HABIHI AJMAINA AMIN.

NAMSHUKURU MOLIWA: KWAHAYA KUYAMALIZA.

KUNIPA NGUVU NAQUWA: NILO NAYO KUYELEZA.

TARIKHI ILIO SAWA : YEO NIMEIMALIZA.

AHMAD MOHAMAD AHMAD AL- JAHADHMY.
LAMU.. 6th AUGUST 1985
P.O.. BOX 36. TELEPHONE 3121 & 3064 LAMU, KENYA

اصل قبيلة الهل الامو وشيوخهم
ينقسم على ثلاثة طوايف وكل فرقة
من هؤلاء تفرعت على اربع فروق

١ كن مت

٢ وافمو

٣ وا اعوان وبمب

وافمو تفرعت اربع فروع

ابوان خمس وموري موري

انقرضو ولم يبقى الا نفرين
ولم ينصبو شايب هم

٢ بون تمان علي

كان شايبهم ابو بكر من عمر
وبعد موته انصبو عبد الله
بن يوسف مدي

٣ المعاويون والخطباء

كان شايبهم عمر بن عمر
على الجميع وبعد موته
كان على الخطباء عبد الله
بن عثمان وبعظم لم يرتضو
ونصبو سعيد بن محمد
والمعاويون نصبو
عبد الله بن ابو بكر المعاوي

٤ بانه غوغ

كان شايبهم شيخ فضل
بن علي وبعد موته نصبو
حسين بن عبد الله وبعد
موته لم ينصبو احد

كن مت تفرعت اربع فروع

١ بانه معلم

كان شايبهم شي صالح بن عبد الرحمن الحسين

٢ بانه مبيكيا منهم الاهاد له
كان شايبهم شريف عبد الله زبير الاهدلي

٣ بوان موني موري

انقرضو ولم يبقى منهم الا نفرين
وهم من المخزومين
ولم ينصبو شيخ بهم

٤ وا اعوان اشنا عشره

كان شايبهم جعفر بن يوسف
وبعد موته لم ينصبو احد

وا اعوان وبمب تفرعت اربع فروع

١ البكري وهم فرعين شيوخهم
جعفر بن عبد الله كبيرة
وعبد الله محمد كبيرة

٢ محمد بن يوسف وهم فرعين
شيوخهم عثمان بن علي
وعمر بن عبد الرحمن

٣ بانه مشوت وزنزير

انقرضو ولم يبقى الا رجل واحد

٤ بوانه مبيكيا وموني موري

منهم الجماضم
اختلفو بعضهم على بعض

ALHAMDU LILLAH NAMSHUKURU MWENYE EZZIMGU

MUSCAT 15-2-1990
19th RAJAB 1410

KAMA SURA NILIVOAZIMIYA INGAWA SIKUTOWA AHADI KUWA KIPATA NAFASI TAJARIBU KUFASIRI BAADHI YAMANENO NAMASHAIRI NAMAFUMBO YALIOMO KATIKA KITABU HIKI NAUTUNGO WAKE CHENYE TAREKH YA LAMU YALIO MAGUMU KUFAHAMIKA KWAKISWAHILI CHASASA TUNACHOTUMIYA SISI KWA WAKATI HUNU. KISWAHILI KINGI KILIYOMO KATIKA KITABU HIKI NI KISWAHILI KILICHOKUWA KIKITUMIWA NA WATU WA LAMU. PATTE. PEMBA. NA MOMBASA WALIOKUWA WAKIISHI ZAMANI HIZO ZAKALE. NAPIYA HATA MASHAIRI WALIOTUMIYA KWANJIYA YAMAFUMBO.

ALHAMDULILLAH NAMSHUKURU MOLA WANGU APASAE KUSHUKURIWA NAKUHIMIDI AMBAE NEEMA ZAKE HAZIWEZI KUHASIBIKA UKAZIPATA ZOTE. NAMSHUKURU KWA NEEMA HINI YAKUNIWEZESHA NAKUNIPA UMRI KAWEZA KUTIMIZA YALE MAKUSUDIO YANGU NILIOWEKA MOYONI MWANGU KUWA KIPATA NAFASI TAFASIRI BAADHI YA MANENO. MOLA MENIPA NAFASI NIMEFASIRI.

I. KAMHADAA= KAMDANGANYA 2.KAMWELEZA=KAMWAMBIYA, KAMPA KHABARI
3. UKO= YUPO. 4.MEPISWA.= HANA AKILI TENA KWASABABU YA UZEE
5. WALIKUYA= WALIKUJA 6. WAPEMA= UPESI, MWANZO, HARAKA.
7. WALIMENA= WALISEMA. 8. WALITAPAKAA= WALIENEYA KOTE.. KILA UPANDE
9. MWATAMU= WATAMU.. I0. KABLA= MBELE, MWANZO. II. mwenyemui= MFALME.

I2.MADAU=MITUMBWI I3. USAHALI=KWA WEPESI. I4. MTEPE= JAHAZI-ZAKIBAJUNI ZINAZOJENGWA KWA KAMBA BILA KUTUMIYA MISUMARI.
I5. KUKOKOTA.=KUBURUTA. I6. KIKONI = KIVUKONI.KUSOWA=KUTWANGA
I8. MTTI=JITI MAALUMU LAKUTWANGIYA NAFAKA.I9.KISHUKA=KITEREMKA.
20. WANGANDU=WANAOVAA DHAHABU.. 2I. KUCHA=KUOGOPA.
22. KIWANRA =PAHALA PAKUTENGEZEA VITU KAMA PANGA AU FURNITURES
23.MJUMB=FUNDI WA VUMA.. 24. KUNOWA=KUTIYA MAKALI SILAHA,
25. NREO=KIBURI,KUJIONA.26. KUYONGOWA=KWENDA KWAKUIRUSHARUSHA.
27.SIWA=BARAGUMU LA SHABA,PEMBE;AU JITI LILILOTEMULIWA NDANI LIKIPULIZWA HUTOWA SAUTI KAMA MGURUMO.
28.ZINGAKII=NIKAWA SIWA LAKIN LILIKUWA KUBWA SANA.
29. WAKFU= KITU KILICHOWEKWA MAKSUDI KUTUMIWA NAWATU MAALUMU.
30. CHAWANYO= MGAWANYIKO,KILICHO GAWANYA,MGAWANYO.
3I.NGOME=GEREZA,JELA,FORT,PAHALI PAKUJILINDA KWA VITA.
32. USIKU WAMANANE=USIKU MKUBWA ULIO ENDELEYA SANA
33.KUMTILIA MIKONONI=KUMPA,KUMKABIDHISHA,KUMTALALAKISHA.
34.MAKUBADHI=MASHIKO MADHUBUTI YENYE NGUVU.MASHIKO SAWSAWA
35.KAKUTA UKUTA=KAONA JENGO,KAONA JENGO LA UKUTA,KIWAMBAZA.
36.KAJIZATITI=KAJIWEKE TAYARI KWA VITA,KAJIFUNGE KWA VITA.
37.TURUDIE=TUREGELEE. 38.TULIPOKOWA=TULIPOFIKA.
39.KUCHA=KUOGOPA.. 40.VUWA=BAHARI ILIOPO KARIBU YA KILIFI.
4I.TAFI=SAMAKI CHAFI.. 42. WAVUWA CHAFI=WAVUVI WA SAMAKI CHAFI..
43.KIROBOTO NAMANYEMA= HAYA YALIKUWA NI MAJINA YA WATUMWA WA MAZRUIY WALIOKUWA WAKIVUA SAMAKI.
44. KWANDAMANA=KUFUATANA.45.MAPEPE=WATU WASIOKUWA NA MAANA
46. MUTIZIENI=YAWAKHUSU NINI? 47.MAHEHE=WAPUMBAVU,MUSOKUWA NAMAANA
48.KUJIONGOWA=KUJITWAZA,KWENDA KWA MARINGO,KWENDA MUKIJIPIGA HUKU NA HUKU KWA KIBURI,MAJIVUNO.
49. ZEZE NA ASHA HAMADI=YALIKUWA NI MAJINA YA WATUMWA WA LAMU.
50. WAKHUBIRINI=WAAMBIYENI,WAJULISHENI,WAPENI KHABARI,WAFAHAMISHE
5I. MLENGA=WANAOJIFANYA MAHODAR,WAJUZI, MASHUJAA.
52. TUMEKONEYA=TUMEFUNGA,TUMEPIGILIA,TUMEFUNGA MADHBUTI.
53.MIDI=KIFUNGIYO CHA MLANGO,TUMBUU YA NDANI YA MLANGO.
54. MAGOGO=MAPANDE YA MITI MANENE NA MAZITO YENYE NGUVU..
55. HIRIMU=WENZETU,WENYE UMRI M'MOJA NA KARNE MOJA NASISI.
56. KUTANGA=KWENDA HUKU NA KULE,KURANDA,KUZUNGUKA KILA UPANDE.
57. KUYUWA=KUJUWA. 58.TATASA PATO=PIGA UTASA KWAKUTATANISHA.
58. UPAMBE=UENEZE,UTENGENEZE.
60. TATANISHA= VURUGA,CHANGANISHA,KOROGA.

61. VIBODOO= VIGINGI VAKUPIGIYA UTASA ZILIZOSOKOTWA KWA NGONGO.
62. UVUMILIZE=UPULIZE,UVUZIYE, 63. MUYUMBE=MJUMBE, MTANGAZAJI, ALIETUMWA KUPELEKA MANENO KWAWATU.
64. MN'REO=MWENYE KIBURI,KIWANDEO,KISIWA CHA KIBURI,JINA LAZAMANI LA KISIWA NA MJI WAKE WA LAMU.
65. YANDAMANE=IFUATANE. 66. MILIO= MISHINDO? MITAKASO.
67. TANDAO=KUENEYA,KUTANGAA,KUSIKIKA SAUTI KILA PAHALA.
68. FURUNGU=JINA LASIWA YA LAMU(AU YAMSHABAKA FURUNGU) MAANA YA FURUNGUAU VURUNGU NIKITU CHENYE SHIMO NDANI
69. KUSI=MAKOFI. 70.WANAWAKE WAPIGAO KUSI(WAPIGAO MAKOFI).
71. ZANDAMANE=ZIFUATANE.72.MAKUNGU=MASIKU KUCHA KUKESHA USIKU.
73.AMBE=ANENE,ASEME,AELEZE.74..USIYAFUMBE=USIYAFICHE,SEMA WAZI,KWELI
75. KIZAZI NA MOYA FUNGU=NDUGU,JAMAA, TULIOZALIKANA,WATU WAMOJA.
76.KUPINDULIYANA=KUGEUZIANA.77.HUZENGELEYANA=HUTEFUTIYANA.
78. MWENDE=MWENZAKE. 79.CHAMBA=KINENA,KISEMA,KIAMBIWA,KIELEZWA.
80. PINDANI=KINYUME.81.ISITWEGEME=ISITUFIKE,ISITUKURUBIYE.
82. ANENENI?=ASEME NINI? 83.KIPILIPILI=LILIKUWA JINA LA MTUMWA.
84.TAKUKUKUTA=TAKUPIGA.. 85.KISIKI=KIGONGO,FIMBO NENE FUPI.
86.TAKANENI=KUTANANI,TEFUTANENI. 87.TUWANDAME=TUWAFUATE.
88.PINDANI=UPINZANI, ISITWEGEME=WASITUSHINDE KWA UMOJA.
89.KWAMIOMO YA BUNDUKI=KWAKUTUMILIWA NGUVU,KWASILAHA YABUNDUKI.
90. CHEO DUNI=KUJIDHALILISHA,KUJIFANYA WANYONGE,KUJIDHARAU.
91.DHAWIRI=NIYA,MAKUSUDIO..92.TUKUZE=TUJIHISHIMU,TUJIWEKE JUU.
93. AUNI=NGUVU,MSAADA. 94. JALIA=MWENYE EZZIMGU ALIE TUKUKA.
95. MKWASI=ALIE JITOSHELEZA,ASIYE MUHITAJIYA MTU KUMSAIDIYA.
96.MFUASI=ANAEFUATA WATU.. 97.MLA= MLAJI,MWENYE KULAWAPUPA.
98.SHOKOWA=KUTUMILIWA NGUVU.. 99. UYAO=ANAKUJA.
100.KIWAMBAWAMBA=KIFUA MBELE,KWA JEURI,KWANGUVWO BILAKUJALI.
101.KUTWEGESHA=KUTUFIKISHA.102.MADHILA=MABAYA,UNYONGE,JEURI.
103.BILA MUHULA=BILA WAKATI, BILA KUNGOJEYA,PASINA MUDA.
104.TASHUKA=TATEREMKA.105. MUTATENDANI?=MUTAFANYIZA NINI?
106.PANI SHAURI=NIPENI SHAURI,NIFAHAMISHENI,NIJULISHENI.
107. MAPEMA..=MWANZO,KABLA,108.MURADI=MAKUSUDIO,LENYEKUFAA.
109.MUWANA WAZIMA=KUFAHAMUO MAMBO,WENYE AKILI, MUWATU WAZIMA.
110.KUTARADADI=KUBADILIKA,KUGEUZA MARA HILI MARA LILE, BILA KUKATA SHAURI LASAWA.
111.KWIMA=KUSIMAMA SAWASAWA.112.SITUUZE=SITUULIZE,HAKIKISHA.
113.MWANAMIZE..=MZEE MWENYEAKILI, JINA LAMAFUMBO LA BWANZAHIDI.
114.TUIZIZE.=TUMEKATAA KWAKUKATA.115.KAWE=KABISA.
116.HELA.=HEBU.117.TUNDA=TIZAMA SANA,FIKIRIYA,ZINGATIYA.
118KWAMBA=KWAKUWA. 119.JIKBI=JOGOO..
120.MTAMBIYA=ANAERANDA. 121. MTASAMBA=ANAEDONA NAKUPARA NAKUCHIMBA ARDHI KWAMAKUCHA.
122. HUUZWA IYE=HUULIZWA VIPI? 123. IYE=VIPI.124AKIWANA=KIPIGANA
125. YANA=JANA 126.YEO=LEO 127. TUNAAPA=TUNAKULA YAMINI,KIAPO.
128.MOLA=MGU 129.DHULI SIYENYETUPATA=HATUTOKUBALI UNYONGE,
130. TULINA= TULIKUWA NAZO. 131. TUTAKUKUTA=TUTAPIGA,TUTAMPIGIYA
132. WATAE WENYE KUZITA=WAZITUMIYE WENYE KUZITUMIYA,WAPIGIYE
133. SAMBE=HATA KAMA,HATA IKIWA. 134. KUTOTA=KUZAMA BAHARINI, KUPOFUKA MACHO,KUWACHONGO.
135.MAYINI=NDANI YA MAJI.. 136. TUKETIZIYE TAYARI=TUMEKAATAYARI.
137.MSHAMARI=BUNDUKI ZILIZOWEKWA TAYARI ZILIZOTIWA RISASI
138.TANA=CHOMBO CHAKUWEKEYA BARUTI.
139.TUKATUZIE=TUMEKATUWA,TUMESUGUWA,TUMESAFISHA. 140.WANA=VIJANA
141. ARI=GHERA,HISHIMA. 142.MAHADAZI=KUDANGANYWA,KUHADAWA,HILA, VITIMVI, UWONGO,UDANGANYIFU
143. YALIPITILE=YAMEKWISHA KUPITA, 144.TUMO=TUKO,TUPO.

145. JAHANE.= KATIKA UTUKUFU. 146. KANAKWAMBA= KAMAKUWA.
147. MUYATAKABO..=MUKITAKA.. 148. MAWANI=MAPIGANO, VITA.
149. KHAFUKANI.=KIBABAIKO, WASIWASI, KITISHO, KICHO, KHOFU.
150. KUFISHWA MOYO.= KUTIWA KHOFU, KUKATISHWA TAMAA.
151. PEPE.=UMEME.. 152.. YANGA=ANGA. 153.KONDO=VITA,MAPIGANO.
154.YUNGA..=JINA LA PATE LAZAMANI. 155.PEFO..=UPEPO.
156. KUSHITADI.=KWENDELEYA, KUTILIA NGUVU JAMBO, 157KUZINGA=KUGEU
158.. WATUMBA.= WATU WASIOKUWA NA MFALME NA MWANAMKE ASIEKUWA NAMU
159.MUHIBU=MPENZI. 160.WARAKA=BARUWA.
161.ZISOKAKA..= KUNI ZISIZOSHIKA MOTO,ZISIZOWAKA.
162. WAOLE=WAPATE KUONA. 163. MBWAWA=MBWAWWITU,WANYAMA WAKALI.
164. WATENDAO=WATENDAVO, WAFANYAVO. 165. MAINDONI= KATIKA=
KUVIZIYE NAKUSAKA.
166.. NDOLE=MAKUCHA.. 167.. KUVIKA=KUTIYA NDANI.
168. NG'ONGO=NYASI ZAKUFANYIA MAFAGIYO
169. KUBELE=WATU HURU,WAUNGWANA, MAKABAILAH.
170.HATUCHI=HATUOGOPI KITU. 171. HATUITUKI=HATUTISHIKI,HATUOGOPI,
HATUNA KHOFU YAKITU CHOCHOTE.
172.. KAE=KALE,ZAMEE. 173.IVU=JIVU.174. NDONI=NJOONI.
175.MUNWE.=MUNYWE.. 176 MATUNGU=MACHUNGU.
177.MUBADILIKE= MUGEUKE. 178.JASADI=KIWILIWILI,BODY,MUILI.
179.. MUWE= MUPATE KUWA.180. TUNGU=SISIMIZI,ANTS,
181. TAI=NDEGE WANAOKULA MIZOGA,MAITI,MAJUMBI.
182.. KWEUSHA=KUONDOSHA EDDA,KWANAMKE KUONDOSHA MSIBA WAKUFILIWA
NA KUME WAKE.
183. KUWAFISIDI=KUWAHARIBU,KUWACHANACHANA, KUWAVURUGA.
184.TUTAWASHUSHA=TUTAWATEREMSHA. 185. HUWALINDA=HUWANGOJEYA.
186. NAKHUDHA PONDA AU PUNDA=JINA LA MATUSI AU LAMAFUMBO KWA
YULE MWENDESHAJI ASIYEKWENDA MWENDO WASAWA,MPUMBAVU..
187.HUTUNDA=HUTIZAMA,HUFIKIRIYA, HUFATISH,KUPELELEZA.
188. MWSAPO=MUKISHA,MUKIFIKA. 189. MWENYE YAI=ALIEKUWA NA YAI.
190. WALIOTOKA TWAANI=WLIOKHUNI,WALIOJITENGA, NA MFALME WAO.
191. BANDAR ABBAS= NI MJI ULIOKO IRAN HIVI SASA.
192. KUTUTENDEYA=KUTUFANYIA.
193. MASHUKIYO YAZAMANI= KAMA TULIVO WATENDEENI ZAMANI.

ALHAMDULILLAHI LEO NIMEMALIZA YALIOKUWA YAHITAJIKA
KUELEZWA ILI KITABU HIKI AMA TARIKH HINI INEZEKANE
KUFAHAMIKA NAKILA MTU MWENYEKUSOMA KITABU HIKI KWA
KISWAHILI IWE USAHALI BILA KUTATIZIKA KWAMANENO
YALIOMO NDANI YAKE, NAIPATIKANE ILE FAIDA YAKE
KAMA NILIVOKUWA NIMEKUSUDIYA. WASSALAM

AHMAD MOHAMAD AHMAD AL- JAHADHMY..
MUSCAT P.O. BOX 2080. SULTANATE OF OMAN
LAMU. P.O.. BOX 36 KENYA

4th JUNE 1991.
20 th DHULKAADA 1411.